

HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA



1. ZABUNI NA.LGA/068/2018/2019/NC/02

ZABUNI YA KUENDESHA CANTEEN YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA


Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imetenga kiasi cha fedha katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2018/2019 kugharamia Shughuli mbalimbali ya maendeleo. Aidha Halmashauri inakusudia pia Kumpata mzabuni atakayeendesha Canteen ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Rorya chini ya utaratibu wa zabuni za kiushindani, Inawatangazia wananchi, makampuni, taasisi mbalimbali, Vikundi vilivyoandikishwa kwamba zabuni inatangazwa ya kuendesha zabuni ya Canteen katika Kipindi cha Mwaka Mmoja kuanzia Tarehe 01/07/2018 hadi 30/06/2019. Hivyo inawaalika wote kuomba zabuni hii.

MASHARTI YA JUMLA YA ZABUNI

- (i) Zabuni ambazo hazitapokelewa na kusomwa hadharani siku ya ufunguzi wa Zabuni hazitafikiriwa na Bodi ya zabuni ya Halmashauri kwa sababu yoyote ile.
- (ii) Vigezo vya tathmini ya zabuni zote vitakuwa kama vilivyoainishwa kwenye tangazo na kwenye nyaraka ya zabuni husika.
- (iii) Kwa maelezo zaidi mwombaji anaweza kununua na kusoma nyaraka za Zabuni toka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa malipo ya Tshs 50,000/= (Elfu Hamsini tu) kwa zabuni, na pesa hazitarudishwa hata kama mwombaji atashindwa Zabuni.
- (iv) Maombi yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na **kuonyesha zabuni iliyoombwa** bila kuwa na alama yoyote ya kuashiria ilikotoka na yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Rorya
S. L. P 250
RORYA

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **26/06/2018** saa **Nne asubuhi** na zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu siku na saa hiyo kuwadia kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya. Waombaji au wawakilishi wao wanaalikwa kwenye zoezi la ufunguzi.


Charles K. Chacha
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
RORYA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RORYA